

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG**

**SIMU NA :027-2530022  
2530042**

**NUKUSHI NA  
:027/2530022  
:027/2530042**



**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),  
S.L.P. 2,  
KATESH-HANANG,  
MANYARA.**

**15/04/2020**

**TANGAZO LA KUKODISHA MASHINE YA KUSAGA NA KUSINDIKA NAFAKA  
(LIMERUDIWA)**

**ZABUNI NA. LGA/059/HQ/2019/2020/NC/10**

Halmashauri ya Wilaya ya Hanang inawatangazia wananchi wote, watu binafsi na Makampuni kuomba Zabuni ya ukodishaji wa mashine ya kusaga na kusindika nafaka. Mashine ipo katika Soko la Kimataifa lililoko Kata ya Endagaw Wilaya ya Hanang' Mkoa wa Manyara.

Mashine ina uwezo wa kusaga na kusindika hadi tani kumi (10) kwa siku

**MASHARTI YA ZABUNI YA KUKODISHA MASHINE**

1. Mwombaji wa Zabuni anatakiwa kulipa ada ya maombi ya Zabuni kiasi cha Tshs 50,000/= benki ya NMB baada ya kupewa Bill na Mhasibu wa Mapato Halmashauri ambayo haitarudishwa hata kama mwombaji wa Zabuni hatateuliwa. Mwombaji wa Zabuni atapewa nyaraka za Zabuni "Tender Document" na Katibu wa Bodi ya Zabuni siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kuanzia tarehe 16/04/2020 hadi tarehe 06/04/2020.
2. Mwombaji atakayeshinda Zabuni ataingia Mkataba wa mwaka moja tu.
3. Mwombaji wa Zabuni anatakiwa ataje bei ya kukodisha mashine ya kusaga na kusindika kwa mwaka mmoja.
4. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atatakiwa kuwa na Leseni ya Biashara ya kusaga na kusindika nafaka na pia atatakiwa kulipia "Subsidiary Licence" kwa Halmashauri ya (W) ya Hanang', atatakiwa kulipa ushuru wa huduma (Service Levy) na awe na risiti ya mashine –"Electronic Fiscal Device" (EFD).
5. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atapaswa kutunza mashine na kuikabidhi kwa Halmashauri ikiwa katika hali nzuri.

6. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atatusika na uharibifu au hasara yoyote itakayojitokeza katika utumiaji na utunzaji wa mashine hiyo wakati ikiwa ndani ya muda wa mkataba.
7. Mwombaji wa Zabuni atatakiwa kulipa fedha zote za ukodishaji wa mashine ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupewa barua ya kukubaliwa.
8. Mwombaji wa Zabuni atatakiwa kulipa gharama zote za umeme na maji katika utumiaji wa mashine atakayokodishiwa.
9. Kama kutatokea kutolewaka au kutolewana katika utekelezaji wa sharti lolote la Mkataba utakaofungwa kati ya Halmashauri na mshindi wa Zabuni pande zote mbili zitakaa na kutatua tatizo kwa njia ya majadiliano. Ikiwa majadiliano yatashindwa kuleta muafaka suala hilo litapelekwa kwa msuluhihi ambaye ni Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tawi la Katesh na ikiwa usuluhihi utashindikana shauri la suala hilo litapelekwa Mahakamani.

Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo:

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG,**


**S.L.P 2,**

**KATESH – HANANG.**

Juu ya bahasa iandikwe **ZABUNI YA UKODISHAJI MASHINE YA KUSAGA NA KUSINDIKA NAFAKA**

10. Mwisho wa kuleta maombi na kupokea maombi ya Zabuni ni siku ya Ijumaa tarehe 06/04/2020 saa 5:00 asubuhi kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang.

- Maombi ya zabuni ambayo hayataletwa na kupokelewa na kusomwa siku ya ufunguzi hayatakubalika.



**BRYCESON P. KIBASSA**

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG**

**NAKALA:**

1. Ofisi ya Katibu Tawala Wilaya Hanang'
2. Watendaji wa Kata - Wajulisheni wananchi katika Kata zenu
3. Watendaji wa Vijiji - Wajulisheni wananchi katika Vijiji vyenu.
4. Mbao za Matangazo